

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM



TAASISI YA RASILIMALI MADINI (MRI)

(ZAMANI CHUO CHA MADINI)

S. L. P 1696, Dodoma

Simu: +255 26 2300472, Fax: +255262963003

Barua pepe: info@mri.ac.tz/principal@mri.ac.tz/registrar@mri.ac.tz

Tovuti: www.mri.ac.tz

NAFASI ZA KUJIUNGA NA MASOMO KATIKA NGAZI YA ASTASHAHADA/STASHAHADA KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Taasisi ya Rasilimali Madini ya Chuo kikuu cha Dar es salaam (Zamani Chuo cha Madini) ni taasisi ya Serikali, yenye uzoefu wa zaidi ya miaka thelathini (30) katika kufundisha wataalamu wa ngazi ya elimu ya kati katika fani za sekta ya Madini, Mafuta na Gesi.

Taasisi ya Rasilimali Madini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Zamani Chuo cha Madini) ina ithibati kamili ya Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE) kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada (NTA level 4 - 6) katika mfumo wa umahili (CBET). Taasisi ya Rasilimali Madini inakaribisha maombi kwa waombaji wenye sifa kuomba nafasi za masomo kwa ngazi ya Astashahada/Stashahada kwa kozi zifuatazo:

- **Jiolojia na Utafutaji Madini** (*Geology and Mineral Exploration*)
- **Uhandisi Migodi** (*Mining Engineering*)
- **Uhandisi Uchenjuaji Madini** (*Metallurgy and Mineral Processing*)
- **Sayansi za Mafuta na Gesi** (*Petroleum Geosciences and Exploration*)
- **Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira** (*Environmental Engineering and Management*)
- **Upimaji Ardhi na Migodi** (*Land and Mine Surveying*)

SIFA ZA KUJIUNGA

- Mwombaji awe na cheti cha kidato cha nne (Form IV) na ufaulu wa masomo manne (4) ya sayansi kwa kiwango cha kuanzia alama D.

JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Waombaji wote wenye sifa wanatakiwa kujaza fomu za maombi na kuzituma Chuoni moja kwa moja. Fomu za maombi zinapatikana katika Taasisi ya Rasilimali Madini Kampasi ya Dodoma na Nzega na katika tovuti ya Chuo: www.mri.ac.tz

Kwa maelezo/msaada zaidi wasiliana nasi kupitia: 0784 893 116 / 0753 858 028.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 03/9/ 2021 saa 9:30 alasiri.

NB:

- Maombi yote yatumwe moja kwa moja kwenda Taasisi ya Rasilimali Madini ndani ya muda uliopangwa
- Fomu za maombi ziambanishwe na nakala halisi ya hati ya malipo ya benki (Pay-in Slip) yenye kiasi cha Tshs. 10,000/= na ilipwe kwa kutumia namba maalum ya malipo (*control number*) iliyotolewa katika fomu za maombi.
- Masomo yataanza mwezi Oktoba, 2021

Fomu za maombi zitumwe kwa:

**NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO-TAALUMA,
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (CHUO CHA MADINI)
S. L. P 35091,
DAR ES SALAAM.**